# FAQ
## Maswali Yanayoulizwa Sana

## na

## Fomu ya Maombi ya 2026



## Je, tarehe ya mwisho ya kutuma ombi ni gani?

Kipindi cha kutuma ombi la YCJF kimefunguliwa hadi tarehe 1 Machi, 2026, 23:59 UTC.

## Je, ninaweza kupata wapi fomu ya ombi?

Hiki hapa kuna kiungo cha fomu yetu ya ombi ambapo unaweza kutuma ombi moja kwa moja kwa kubofya wasilisha kwenye lugha unayopendelea. Tovuti yetu ya maombi – https://youthclimatejusticefund.submittable.com/submit – inapatikana katika Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kihindi, Kireno, Kihispania na Kiswahili.

## Je, ninahitaji kufungua akaunti ili kutuma ombi?

Unapotembelea fomu ya ombi na kubofya wasilisha, utaombwa kufungua akaunti ya Submittable kwa kutumia anwani yako ya barua pepe ya kibinafsi, kuunda nenosiri na kuweka jina lako la kwanza na jina la mwisho.




Ukimaliza, utapokea barua pepe kutoka kwa Submittable ikikuomba uthibitishe anwani yako ya barua pepe. Bofya kiungo ili kuthibitisha na unaweza kuanza kujaza fomu yetu ya ombi.

YCJF

## Nilijisajili kwenye Submittable lakini sikupokea barua pepe yangu ya uthibitishaji?

Inaweza kuchukua hadi dakika 15 ili upokee barua pepe ya uthibitishaji. Tafadhali onyesha upya kikasha chako na uangalie folda zako zote (ikiwa ni pamoja na barua taka, masasisho, n.k) ili kuhakikisha kuwa hukosi barua pepe hiyo.

## Je, ninaweza kuhifadhi ombi langu na kuendelea baadaye?

Ndiyo.Unaweza kuhifadhi majibu yako na kurudi kwa ombi lako baadaye. Kumbuka kubofya hifadhi unapojibu swali jipya. Ikiwa simu au kompyuta yako inaishiwa na chaji, data ya mtandaoni au unahitaji kuacha kujaza fomu ili kuhudhuria jambo la dharura, bofya tu hifadhi na utapokea kiungo kwenye barua pepe yako ambacho unaweza kutumia ili kuendelea na ombi lako baadaye. Bofya tu kitufe cha kuwasilisha baada ya kukamilisha kujaza fomu.

## Je, inachukua muda kiasi gani kujaza fomu ya ombi?

Tunakadiria kati ya dakika 30 hadi 60 ili kukamilisha ombi lako.

## Je, ninaweza kutuma ombi langu kupitia barua pepe?

Njia zinazopendekezwa za kutuma ombi ni kupitia jukwaa letu la kutuma ombi mtandaoni ambalo unaweza kufikia hapa: https://youthclimatejusticefund.submittable.com/submit. Katika hali ambapo waombaji hawawezi kufikia jukwaa la maombi mtandaoni, wanaweza kuwasiliana na Kamati zetu za Kanda kupitia ask@ycjf.org ili kushirikiana nao kutafuta suluhisho la kuwasilisha maombi yao

## Je, ni nani anayeweza kutuma ombi kwa ajili ya Youth Climate Justice Fund?

Vikundi vinavyoongozwa na vijana vinavyotetea haki ya hali ya hewa, ambavyo ni jumuishi, vinazingatia mtazamo wa makutano ya changamoto (intersectional), na vinakuza hatua za pamoja katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.Tafadhali soma vigezo vyetu hapa: https://ycjf.org/how-to-apply

## Je, ninahitaji kusajiliwa kisheria?

Hapana, usajili rasmi au wa kisheria hauhitajiki.

YCJF

## Je, Mtu Binafsi anaweza kutuma maombi ya ufadhili?

Lengo letu ni kufadhili uundaji wa harakati na waandaaji wa ngazi ya jamii.
Hii inamaanisha kuwa mtu binafsi anaweza kutuma ombi ikiwa kazi yake ni sehemu ya/inasaidia kikundi kilichotambuliwa cha haki ya hali ya hewa.

## Tumeanzisha shirika au kikundi chetu hivi karibuni—je, bado tunaweza kuomba ufadhili ingawa ndio tumeanza?

Ndiyo! Kila shirika, kikundi, au mkusanyiko unaoongozwa na vijana unaweza kuomba, bila kujali kama umeanzishwa hivi karibuni au una uzoefu wa miaka kadhaa.

## Je, ninaweza kutuma maombi zaidi ya moja?

Hapana. Kwa sababu ya idadi kubwa ya maombi, tunapendekeza waombaji watume ombi moja kwa kila kikundi, shirika au mtu binafsi.Unaweza kueleza miradi yako katika fomu ya ombi.

## Kikundi changu hakina bajeti ya kila mwaka.

Bajeti ya mwaka sio hitaji. Ikiwa kikundi chenu ni kipya kisicho na bajeti ya kila mwaka, chagua 'hapana' unapojibu swali hilo.

## Je, ninawezaje kufikia na kupakia bajeti kwa kutumia kiolezo kilichotolewa?

Unaweza kupakia bajeti yako katika muundo unaopendelea. Pia tumetoa kiolezo cha bajeti katika fomu ya maombi kwenye Submittable ambacho unaweza kutumia kama mwongozo. Pakua kiolezo, kijaze na upakie katika sehemu ya bajeti ya fomu ya maombi ya mtandaoni.

YCJF

## Sipati eneo langu kwenye orodha, nifanye nini?

Mgawanyiko wa kikanda sio kamili. Tunakuhimiza kutuma maombi kwa kutumia eneo ambalo liko karibu na lako. Kwa mfano, ikiwa unatoka Balkan Magharibi, unaweza kuchagua Ulaya na Asia ya Kati. Tafadhali rejelea ramani hii kwa mwongozo.

## Je, ninaweza kutarajia kujua matokeo ya ombi langu lini?

Tutakuwa tukikagua maombi yanapokuja. Kwa sababu ya idadi kubwa ya maombi, tunatarajia kuwajulisha waombaji wote kuhusu uamuzi wetu kufikia katikati ya 2026.

## Je, mradi wangu ukichaguliwa, nitapokea pesa lini?

Ruzuku inapotolewa, tunafanya kazi kwa karibu na kila mshirika anayepewa ruzuku, kwa kuzingatia muktadha na mahitaji yao, ili kutoa pesa haraka iwezekanavyo.

## Ningependa kushirikiana na YCJF ili kusaidia mradi wangu

Wapokeaji wetu wa ufadhili ni washirika wetu. Hatua ya kwanza katika ushirikiano ni kuomba ufadhili wetu. Tafadhali tuma ombi kwenye jukwaa letu na ufafanue mahitaji yako ya ushirikiano chini ya maelezo ya mradi

## Sikuweza kupata Mwezeshaji wa Kikanda wa kanda yangu kwenye tovuti yenu, nifanye nini?

Kwa sasa tuna Kamati 6 za Kanda zinazoshughulikia: Asia Kusini, Asia-Pasifiki, Marekani Kaskazini, Ulaya, Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, Amerika ya Kusini na Karibiani, na Mashariki ya Kati na Kaskazini mwa Afrika. Wanachama wa Kamati ya Kanda si lazima wawe wawakilishi wa kanda yote, bali ni watu binafsi wanaoweza kushirikiana kusaidia washirika wetu wapokeaji wa ufadhili katika kanda hiyo. Tafadhali rejelea ramani iliyo kwenye fomu ya maombi ili kupata nchi/kanda yako na tutamteua Mwezeshaji wa Kanda anayefaa kusaidia.

## Sihitaji ufadhili. Je, naweza kuomba usaidizi wa kuimarisha uwezo?

Kama huhitaji ufadhili lakini unavutiwa na mpango wetu wa kuimarisha uwezo, tuma barua pepe kwa ask@ycjf.org ukielezea aina ya maeneo ya uwezo ambayo ungependa kuimarisha.

YCJF

# Maswali yanayoulizwa sana kuhusu YCJF

## Je, tunamaanisha nini kwa kusema 'kushughulikia hali ya hewa na haki ya kijamii na kimazingira'?

Tunamaanisha suluhisho, kampeni, na miradi inayoshughulikia mgogoro wa tabianchi kwa kushirikiana kukabiliana na ukosefu wa usawa, unyonyaji na ukandamizaji, huku ikiimarisha nguvu, usawa na haki ndani ya jamii.

## Tunamaanisha nini kwa kusema "inayoongozwa na vijana"?

Tunaamini kuwa neno "vijana" lina maana na muktadha mbalimbali kulingana na mitazamo na mazingira tofauti duniani. Tunaamini kuwa kulinganisha kati ya vijana wazima chini ya umri wa miaka 35 ambao wanadhalilishwa au kutengwa kutokana na tabaka, kabila, utambulisho wa Watu Asili, jinsia, n.k., na wanaharakati wachanga ambao pia wanakabiliwa na vizingiti kama hivyo vya kimuundo, ni jambo la msingi.

## Je, mafunzo ya ushirikiano kati ya vijana kupitia Kuimarisha Uwezo ni nini?

Tunashirikiana na mtandao wetu kutoa mafunzo ya ushirikiano kati ya vijana kuhusu ujuzi muhimu unaohitajika kwa ujenzi wa harakati, kama vile Kampeni na Mawasiliano, Usimamizi na Uongozi, Uelewa wa Kifedha na Ukusanyaji wa Fedha, Utawala na Uendeshaji na Usimamizi wa Miradi.

## Je, YCJF hufadhiliwa vipi?

Tunapata usaidizi kutoka kwa watu binafsi na mashirika ya hisani – badala ya kampuni binafsi au zinazoorodheshwa kwenye soko. Hatukubali ufadhili kutoka kwa mtu yeyote ambaye haendani na kanuni na maadili yetu

## Tunaweza kuomba hadi $20,000 na $40,000 USD, lakini je, tunaweza kutuma ombi hata kama kikundi chetu kinahitaji ufadhili zaidi?

Katika hatua hii, vikundi vya kieneo vinaweza kuomba hadi $20,000 ilhali vikundi vya kitaifa vinaweza kuomba hadi $40,000. Mnaweza kutuma ombi ikiwa mahitaji yenu ya jumla ya ufadhili yanazidi kiasi hiki

YCJF

## Sisi ni kikundi kinacholenga kikanda au kimataifa. Je, tunaweza kutuma maombi?

Wito wetu wazi wa 2026 ni kwa vikundi vya kitaifa na vya kieneo pekee. Ikiwa shirika lenu ni la kikanda/kimataifa, tafadhali tuandikie ujumbe kwa ask@ycjf.org.

*Tafadhali soma kwa makini na ututumie barua pepe tu ikiwa maswali yako hayajajibiwa. Tafadhali kumbuka kuwa hatutajibu barua pepe zenye maswali ambayo tayari yamejibiwa hapa au kwenye tovuti yetu.

# Fomu ya Maombi ya 2026

*Tafadhali kagua maswali ya Ombi la 2026 kabla ya kuwasilisha kupitia Submittable.

## SEHEMU YA A – VIGEZO VYA UTIMIZAJI WA MASHARTI

### Je, kikundi chenu ni shirika/kikundi kinachoongozwa na vijana?

Ndiyo/Hapana*

*Tafadhali kumbuka kwamba ikiwa shirika/kikundi chenu hakiongozwi na vijana, hamjatimiza masharti ya kutuma ombi letu la ruzuku.

YCJF

## Je, kikundi chenu kimesajiliwa kisheria na kina akaunti rasmi ya benki ya kupokea ruzuku? (Tafadhali kumbuka kuwa vikundi vilivyosajiliwa na visivyosajiliwa vinatimiza masharti ya kutuma maombi kwa YCJF)

Ndiyo / Hapana

## Ikiwa hakijasajiliwa, je, mna mfadhili wa kifedha au shirika mbia ambalo linaweza kupokea ruzuku kwa niaba ya kikundi chenu ikiwa mtafaulu?

Ndiyo / Hapana

## Je, kikundi chenu kiko katika eneo gani?

(Waombaji kutoka nchi zenye mapato ya juu wanapaswa kuwa wanatoka katika makundi ya wachache au makundi ambayo hayajahudumiwa ipasavyo ili kuzingatiwa kwa ufadhili. Vikundi vinavyoangazia shughuli za kimataifa pekee bila kazi yoyote ya jumuiya havijatimiza masharti ya kutuma maombi).*

- Asia ya Mashariki na Pasifiki
- Ulaya na Asia ya Kati
- Amerika ya Kusini na Karibi
- Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini
- Amerika ya Kaskazini
- Asia ya Kusini
- Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara

*Tafadhali rejelea ramani iliyo hapa chini ili kutambua eneo lenu




YCJF

## Je, uongozi wa kikundi chenu unajihusisha na mojawapo ya yafuatayo:

- Kinaongozwa na jamii asili
- Kinaongozwa na womxn (ikiwemo uongozi wa wanawake, watu wasiojitambulisha kwa jinsia ya kiume au kike, n.k.)
- Kinaongozwa na LGBTQI2S+
- Kinaongozwa na wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi
- Kinaongozwa na wafugaji/wakulima vijana
- Kinaongozwa na watu wa rangi / wachache kikabila
- Kinaongozwa na watu wenye ulemavu
- Kinaongozwa na wakimbizi/wahamiaji/watu waliokimbia makazi yao ndani ya nchi
- Kinaongozwa na watoto
- Nyingine (ikiwa utambulisho wa uongozi wenu haujaorodheshwa hapo juu, tafadhali eleza kwa maneno yenu mwenyewe asili ya uongozi wenu)

## Je, upeo wa shughuli za shirika/kikundi chenu ni upi?

- Kiwango cha eneo (Jumuiya moja/ eneo la chini ya taifa, mfano wilaya, jimbo, mkoa au jiji)
- Kiwango cha kitaifa (Nchi nzima, katika jumuiya na maeneo mbalimbali ya chini ya taifa)
- Kiwango cha kieneo (Nchi mbili au zaidi ndani ya eneo au kanda maalum)
- Kiwango cha kimataifa (Nchi katika maeneo mengi au duniani kote)

## Je, watu waliopo katika nafasi za kufanya maamuzi katika kundi lenu wana umri gani?

- 19 na chini yake
- 20 - 24
- 25-29
- 30 - 35
- 35 na zaidi
- Mwingine (ikiwa mna uongozi wa vizazi mbalimbali, tafadhali bainisha muundo wake" kwa wale wenye uongozi unaojumuisha makundi tofauti ya umri.

## Je, angalau 75% ya jamii inahudumiwa na kikundi chako ina chini ya umri wa miaka 35?

Ndiyo / Hapana

## Je, kazi za kundi lenu zinalenga kuwawajibisha watunga sera?

*Hii inaweza kujumuisha (lakini siyo tu) kampeni na shughuli zinazolenga kushinikiza au kusaidia watoa maamuzi kutekeleza ahadi zao za hali ya hewa na mazingira.

Ndiyo / Hapana

YCJF

## Je, kazi ya kikundi chenu inalenga katika kuinua ari ya kuchukua hatua za usawa na za haki kuhusu mabadiliko ya tabianchi?

*Hii inaweza kujumuisha (lakini siyo tu) shughuli zinazoshughulikia ukosefu wa uharaka katika hatua za hali ya hewa na mazingira kwa kuwasilisha suluhisho bunifu na makini zinazoongozwa na jamii za asili/wenyeji, pamoja na mbinu zinazoweza kupanuliwa na serikali, biashara na jamii kwa ujumla.

Ndiyo / Hapana

## Je, kazi za kikundi chenu zinalenga kukuza uongozi wa aina mbalimbali unaojengwa juu ya hatua za haki na usawa katika masuala ya hali ya hewa?

*Hii inaweza kujumuisha (lakini sio tu) shughuli zinazojenga uongozi wa vijana katika nguvu ya pamoja ya kutekeleza hatua za hali ya hewa, pamoja na njia za vitendo za kuimarisha nguvu ya jamii na nguvu ya pamoja katika utekelezaji wa hatua za hali ya hewa.

Ndiyo / Hapana

## Je, kikundi chenu kina bajeti ya kila mwaka?

Ndiyo / Hapana

## Kama ipo, bajeti hiyo ya mwaka ni ya kiasi gani?

(Wito wazi wa YCJF huweka kipaumbele kwa vikundi vya mashinani vinavyoibuka. Tunatambua kwamba vikundi vilivyoanzishwa vinavyoongozwa na vijana vilivyo na bajeti ya kila mwaka ya zaidi ya $100,000 vinaweza kukabiliana na changamoto katika kuendeleza kazi zao. Ikiwa kikundi chenu kiko katika kitengo hiki na unaamini kuwa kazi yenu inaendana na malengo yetu, tafadhali wasiliana nasi kupitia ask@ycjf.org)

- 0 - 10,000
- 10-25,000
- 25-50,000
- 50-100,000
- 100,000 na zaidi

*Kiwango cha bajeti katika USD

## SEHEMU YA B - MAELEZO YA KIKUNDI / MRADI

Ikiwa unahitaji usaidizi wowote wa kukamilisha ombi lako tafadhali wasiliana na Viongozi wetu wa Maeneo kupitia ask@ycjf.org

### Jina la kikundi chenu

Jibu fupi

### Je, eneo la msingi la kazi ya kikundi chako ni lipi?

Jibu fupi (orodha ya maeneo)

### Jina la Kiongozi wa Pendekezo
*Mtu anayetuma ombi

Jibu fupi (jina kamili la kiongozi)

### Nafasi ya Kiongozi wa Pendekezo katika kikundi

Jibu fupi (jukumu)

### Tarehe ya Kuzaliwa kwa Kiongozi wa Pendekezo

DD/MM/YYYY

### Njia ya mawasiliano ya kikundi (barua pepe/WhatsApp, signal/simu)

Jibu fupi (jumuisha zote hapo juu ikiwezekana)

YCJF

## Je, lengo la msingi na dira ya kimkakati ya kikundi chenu ni ipi?

Jibu fupi (maneno yasizidi 100)

## Je, eneo la msingi la kikundi chenu ni lipi?

- Bioanuwai na asili
- Mzunguko wa uchumi na taka
- Urekebishaji na kujenga uimara
- Hasara na uharibifu
- Mifumo ya chakula na maji
- Miji na mazingira ya mijini
- Afya na ustawi
- Nishati na mpito wa haki
- Teknolojia na Ubunifu
- Nyingine (Ikiwa mpango wenu unalenga mada ambayo haijaorodheshwa, tafadhali eleza mada kuu ya kazi yenu kwa maneno yenu wenyewe)

## Eleza kwa ufupi mradi/shughuli kuu ambayo kikundi kinatafuta usaidizi.

Jibu refu (Eleza tatizo mlilotambua na kushughulikia hapo awali ambalo linaweza kuwa linahusiana au halihusiani, na jinsi uzoefu huo unavyoweza kuboreshwa na ruzuku hii)
(Isizidi maneno 200 - Hii inaweza kuwa kitu chochote kutoka kwa shughuli maalum za kikundi chenu hadi vipaumbele vyenu kwa miaka iliyopita)

## Je, timu imefanikisha nini kufikia sasa na ruzuku hii itaendeleza vipi mafanikio yenu yaliyopo, ikiwa yapo?

Jibu fupi
*Eleza kwa ufupi tatizo ambalo kikundi chenu kilitambua na kushughulikia hapo awali ambalo linaweza kuwa linahusiana au halihusiani, na jinsi uzoefu huo unavyoweza kuendelezwa kupitia ruzuku hii.

YCJF

## Je, mafanikio haya ya awali na mradi wa sasa yanaendana vipi na malengo ya YCJF ya kuwawajibisha watunga sera, kuongeza ari kwa hatua za haki na usawa katika masuala ya hali ya hewa na mazingira na kukuza uongozi wa vijana uliojikita katika nguvu za jamii?

Jibu fupi
*Isizidi maneno 100.

## Orodhesha washirika wowote ambao kikundi chako kinashirikiana nao.

Jibu fupi
*Isizidi maneno 100.

## Je, kikundi chenu kinajumuisha vipi au kinapanga kujumuisha vipi kanuni za haki, utofauti na ujumuishaji katika juhudi zilizoelekezwa katika kusaidia makundi ambayo hayajahudumiwa ipasavyo?

Jibu fupi
*Isizidi maneno 100.

## Je, maono ya kikundi chenu katika miaka 3 kutoka sasa ni yapi?

Jibu fupi
*Isizidi maneno 100.

YCJF

## Je, mnaomba kiasi gani cha ufadhili? (Vikundi vya kieneo vinaweza kutuma maombi ya hadi $20,000, vikundi vya kitaifa vinaweza kutuma maombi ya hadi $40,000)

Jibu fupi

## Je, mtatumia pesa hizi kufanya nini? Tafadhali pakia bajeti yenu

Tafadhali pakia bajeti yenu kwa kutumia kiolezo hiki kama mwongozo.

## Je, ni uwezo gani na mahitaji ya kuimarisha shirika ambayo kikundi chenu kinahitaji kama ziada ya ufadhili? *Tunawezaje kuwasaidia zaidi ya ruzuku hii

Jibu fupi (Tunawezaje kuwasaidia zaidi ya ruzuku hii)

## Ili kutusaidia kuelewa vizuri kikundi chenu na kazi mnayofanya;

a. Tafadhali wasilisha viungo vya kazi yenu yaani Linkedin, Facebook, Instagram, tovuti n.k.

b. Zaidi ya hayo, tafadhali wasilisha hati au faili zozote zinazohusiana, kama vile ripoti za miradi, ripoti za kila mwaka, machapisho, maelezo ya hadithi, au rekodi za sauti/video za shughuli za hivi karibuni.

## Ninakubaliana na sera ya YCJF ya kuhifadhi taarifa zilizotolewa katika maombi haya kwa mzunguko wa ufadhili wa YCJF 2026.

☐

YCJF